JEDWALI LA MALIPO YA ADA.

DARASA	I	II	III	IV	V	VI	VII
ADA	2,800,000	2,800,000	2,800,000	2,800,000	2,800,000	2,800,000	2,800,000
AWAMU YA 1 (DEC 2021)	1,200,000	1,200,000	1,200,000	1,300,000	1,300,000	1,300,000	1,700,000
AWAMU YA PILI (APRIL 2022)	600,000	600,000	600,000	600,000	600,000	600,000	600,000
AWAMU YA 3 (JUNE 2022)	500,000	500,000	500,000	500,000	500,000	500,000	500,000
AWAMU YA 4 (SEPT 2022)	500,000	500,000	500,000	400,000	400,000	400,000	

UFAFANUZI WA MALIPO YA ADA:

- Ada ya masomo kwa mwaka ni **Tshs 2,800,000/=** italipwa kwa awamu nne kama ilivyoanishwa kwenye jedwali hapo juu.
- Ada ilipwe katika akaunti maalum za Ada nazo nia

AKAUNTI ZA MALIPO YA ADA		
BENKI NBC	**BENKI** AMANA	**BENKI** KCB
JINA LA AKAUNTI	**JINA LA AKAUNTI**	**JINA LA AKAUNTI**
IBUN JAZAR ISLAMIC ENGLISH MEDIUM PRIMARY SCHOOL	IBUN JAZAR ISLAMIC ENGLISH MEDIUM PRIMARY SCHOOL	IBUN JAZAR ISLAMIC ENGLISH MEDIUM PRIMARY SCHOOL
NAMBARI YA AKAUNTI	**NAMBARI YA AKAUNTI**	**NAMBARI ZA AKAUNTI**
048132000088	001120310750001	3300618819

JEDWALI LA MICHANGO MINGINE:

DARASA	I	II	III	IV	V	VI	VII
Vitabu & stationary	130,000	130,000	130,000	150,000	150,000	150,000	150,000
Sare za shule	140,000	140,000	140,000	140,000	-	-	-
Mitihani				70,000			100,000
Godoro, kava, shuka na neti	110,000						
Jumla	**380,000**	**270,000**	**270,000**	**360,000**	**150,000**	**150,000**	**250,000**

UFAFANUZI WA MALIPO YA MICHANGO MINGINE:

- Michango mingine inatofautiana kati ya darasa na darasa.Inalipwa mwanzoni mwa mwaka katika akaunti tofauti na akaunti ya malipo ya Ada na kuleta risiti siku ya kufungua shule.
- Wanafunzi wanao hamia wote wanapaswa kulipia michango yote (isipokuwa mitihani ni kwa madarasa maalum).
- Akaunti ifuatayo hapo chini ndiyo itatumika kufanya malipo ya michango mingine

Benki: **AMANA .**
Jina la akaunti: **IBUN JAZAR ISLAMIC ENGLISH MEDIUM PRIMARY SCHOOL LOWER OTHER.**
Nambari ya akaunti: **001120310750004.**

ZINGATIA:-

- Mlipaji wa ada anapaswa kuhakikisha anaandika majina matatu ya mtoto anae mlipia na darasa lake pamoja na kuleta risiti hiyo shuleni siku ya kufungua shule.
- Malipo ya ada na michango mingine yakishalipwa hayarudishwi.

2022

UFAFANUZI WA MALIPO

Kwa wanafunzi wanaohamia madarasa mengine watalazimika kulipia PESA YA SARE Tshs 140,000 na pesa ya Godoro, kava, shuka, neti Tshs 110,000 katika orodha ya michango mengine.

- Awamu za ada zitalipwa kama ifuatavyo;
  a) Awamu ya kwanza italipwa Mwezi Desemba 2021.
  b) Awamu ya pili italipwa wakati wa kufungua shule kutoka likizo ya nusu muhula wa kwanza (Midterm).
  c) Awamu ya tatu italipwa wakati wa kufungua shule baada ya likizo ya Muhula wa pili.
  d) Awamu ya nne ni wakati wa kufungua shule likizo ya nusu muhula wa pili (Midterm).

ZINGATIA

MALIPO YA ADA PAMOJA NA MALIPO MENGINE YAKISHALIPWA HAYATARUDISHWA

- Risiti ya malipo ya benki (Bank Pay-in-slips) ni lazima iwasilishwe kwa muhasibu ndani ya siku na saa za kazi, hayatatambulika malipo ambayo risiti yake haikuwasilishwa kwa muhasibu.
Ni kosa kufanya malipo mkononi (Cash Payments). Shule haitayatambua na haitawajibika kwa malipo yoyote yalolipwa mkononi.
Hatapokelewa mwanafunzi ambaye hatatimiza kiwango cha ada cha awamu husika.

- **Shule itafunguliwa Januari 10, 2021**, watoto wataanza kupokelewa saa 07:00 Mchana mpaka saa 11:30 Jioni, hatapokelewa mtoto atakayefika nje ya muda huo.

IBUN JAZAR Islamic PRIMARY SCHOOL



FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

HEADTEACHER 0677 883311
SECOND HEADTEACHER 0677 099991
ACCOUNTANT 0677 883322

E:mail: headteacher@ibunjazar.or.tz

Web: www.ibunjazar.or.tz

1.0 UTANGULIZI

Shule ya msingi IBUN JAZAR ni shule ya kiislamu inayotoa elimu ya msingi, elimu ya dini ya kiislamu na kuhifadhisha Qur'an.
Shule ipo katika mji wa Vikindu, Wilaya ya Mkuranga mkoa wa Pwani na ni ya bweni kwa wavulana na wasichana.

1.1 DHAMIRA YA SHULE

Shule ya msingi IBUN JAZAR ni shule bora inayodhamiria kumuendeleza mtoto kitaaluma, kimwili na kiroho ili kujenga jamii yenye wasomi wenye maadili mema na wawajibikaji.

2.0 MAHITAJI YA SHULE

2.1 Mahitaji ya kiofisi

Mzazi anatakiwa kuleta vitu vifuatavyo wakati wa kuripoti shuleni

i. Picha mbili (2) za wazazi au walezi
ii. Picha (2) za mwanafunzi
iii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iv. Faili ya plastiki moja (spring file)

2.2 Mahitaji ya bweni

i. Tranka la kuhifdhia vifaa bwenini
ii. Begi la kuhifadhia madaftari.
iii. Taulo rangi yoyote isipokuwa nyeupe
iv. Kandambili
v. Sabuni ya unga kilo 3 na miche mitatu kwa kila muhula.
vi. Miswaki nusu dazeni na dawa ya meno nusu dazeni kwa kila muhula.
vii. Sabuni ya kuogea (medicated soap) dazeni moja.
viii. Sahani ya bati yenye patisheni.
ix. Vikombe viwili vya mfupa (si plastiki) kwa kila muhula.
x. Nguo za ndani pea 4 kwa kila muhula,
xi. Vikata kucha (nail cutters) viwili (2).
xii. Nguo za michezo (trauck suits) – (Drs 1 -3, Buluu) (Drs 4 – 5, Nyekundu), (Drs 6 – 7, Njano)
xiii. Kanzu nyeupe (2) kwa wavulana na baibui nyeusi (2) zisizo na marembo kwa wasichana.
xiv. Soksi pea zaidi ya tatu.
xv. Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na kamba.
xvi. Ndoo moja na kopo la kuogea.
xvii. Sweta rangi ya bluu.
xviii. Rangi ya viatu kopo mbili pamoja na brashi za kung'arishia kubwa na ndogo.

3.0 MWENENDO NA MAADILI

• Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu maadili yote yadini ya kiislamu.
• Mwanafunzi anatakiwa kuwa mtiifu kwa walimu viongozi, wafanya-kazi na wanafunzi wenzake.
• Mwanafunzi anatakiwa kuwa mtulivu darasani na katika mazingira yote ya shule kwa ujumla.
• Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi wa mwili, mavazi na mzingra yake yote yanayomzunguka.
• Mwanafunzi haruhusiwi kufuga kucha, kupaka rangi, hina au piko, kuvaa nguo za kubana, kuweka nywele bandia, kuvaa pete, mkufu, bangili n.k
• Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vifaa vya kieletroniki kama simu ya mkononi, redio, kamera, jagi la kuchemshia maji n.k
• Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule atakaposafiri kuja shule au kurudi nyumbani kwao.

3.1 Kanuni za bweni

• Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya shule isipokuwa kwa kibali maalum (gate pass)
• Mwanafunzi atatembelewa kwa mwezi mara moja kulingana na kalenda ya shule inavyo onesha.
• Mwanafunzi anatakiwa ajipambe na sifa nzuri pamoja na madili ya kiislamu muda wote akiwa bwenini.
• Mwanafunzi anatakiwa awe msafi pamoja na kuhakikisha usafi wa mazingira yanayozunguka bweni lake na shule kwa ujumla.

3.2 Makosa ya kinidhamu na adhabu

3.2.1 Makosa yanayopelekea kufukuzwa shule

Makosa yafuatayo yanaweza kupelekea mwanafunzi kufukuzwa shule;

- Wizi
- Utumiaji wa vilevi
- Kupigana
- Kufanya uasherati, ubakaji, ushoga na uzinzi.
- Kugoma, kuchochea mgomo na kugomea adhabu.
- Kupata, kusababisha au kutoa mimba.
- Kuruka ukuta wa shule.

TANBIHI:

Shule haitawajibika kurudisha kiasi chochote cha ada iliyokwishalipwa iwapo mwanafunzi atafukuzwa kwa moja ya makosa tajwa hapo juu au kosa lingine la kinidhamu.

3.2.2 Makosa yanayopelekea adhabu kali au kusimamishwa kwa muda

Mwanafunzi ataadhibiwa au kusimamishwa kwa muda (suspension) akikutwa na makosa yafuatayo;

• Utoro
• Matusi
• Kuchelewa darasani, mstarini, msikitini n.k
• Kukaa faragha baina ya msichana na mvulana
• Kutishia usalama wa walimu, wafanyakazi au wanafunzi wenza.
• Udanganyifu (kama kusingizia ugonjwa)

4.0 MASOMO NA TAALUMA

Mwnafunzi anatakiwa kufanya bidii katika masomo yake yote kwa ujumla kwa kuhudhuria darasani, kujisomea pamoja na kushirikiana kwa ukaribu na walimu wake.

4.1 Masomo yanayofundishwa

1 . Hisabati
2. Kiingereza
3. Kiswahili
4. Sayansi
5. Maarifa ya jamii
6. Uraia na Maadili
7. Stadi za Kazi
8. Maarifa ya Uislamu
9. Lugha ya Kiarabu
10. Kusoma na kuhifadh Quran
11. Kompyuta

4.2 Lugha ya kufundishia

Masomo yote yatafundishwa kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa masomo ya lugha ya Kiarabu, Kiswahili na maarifa ya uislamu.

4.3 Lugha ya Mawasiliano

Lugha ya mawasiliano shuleni ni Kiingereza na kiarabu tu. Mwanafunzi anatAkiwa kutumia lugha hizo muda wote awapo shuleni.

4.4 Wastani wa kufaulu

Mwanafunzi anatakiwa kufaulu kwa wastani usiopungua 61 katika masomo yote.

5.0 MEDICAL CHECK UP

Wanafunzi wote watalazimika kucheki afya zao katika hospitali ya shule. Mwanafunzi atakubaliwa na kupokelewa baada ya shule kujiridhisha na mwenendo wa afya yake.

6.0 **BIMA YA AFYA**: Mzazi anapaswa kulipa shilingi 50,400/- kwa ajili ya bima ya NHIF au kuja na kadi ya bima hiyo.

7.0 MALIPO YA ADA

• Ada inawezekana kulipwa yote kwa mkupuo mmoja au kwa awamu nne.
• Awamu za ada pamoja na malipo mengine ya lazima yameainishwa katika jedwali la malipo.

TANBIHI:

• Malipo ya safari za kimasomo na programu maalumu hayakujumuishwa katika malipo. Malipo hayo yatafanyika kwa mujibu wa maelekezo yatakayotolewa na shule kwa wazazi wa wanafunzi wa madarasa husika.

• Malipo ya michango mingine yalipwe benki kwa risiti tofauti na risiti ya ada na iwasilishwe kwa muhasibu. (Hatapokelewa mwanafunzi ambaye hajakamilisha malipo hayo wakati wa kufungua shule Januari).